

# Utangulizi

Tanzania ni mionganini mwa nchi zinazoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi. Athari za mabadiliko ya tabianchi zimeonekana katika sekta mbalimbali za uzalishaji nchini ikiwemo sekta za Kilimo, Mifugo, Maji, Nishati, Maliasili, Miundombinu na Usafirishaji. Athari hizi ni pamoja na matukio ya ukame; mafuriko; maporomoko ya udongo; ongezeko la joto; kuibuka na milipuko wa magonjwa ya mazao, mifugo na binadamu; na uwepo wa viumbe vamizi. Jamii maskini hasa za vijijini huathiriwa zaidi na mabadiliko ya tabianchi.

Katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Serikali kuitia Ofisi ya Makamu wa Rais inaratibu utekelezaji wa Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia Mifumoikolojia Vijijini.

Mradi huu ni wa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia 2018 hadi 2022 na umefadhiliwa na Mfuko wa Mazingira Duniani (Global Environment Facility – GEF) kwa gharama ya Dola za Marekani 7,571,233 sawa na shilingi 17,413,835,900.

Mradi unatekelezwa katika Wilaya za Mvomero (Morogoro), Simanjiro (Manyara), Kishapu (Shinyanga), Mpwapwa (Dodoma) Tanzania Bara na Kaskazini A - Unguja, upande wa Zanzibar. Maeneo ya Mradi yalichaguliwa kwa kuzingatia maeneo yenye ukame yenye jamii za wakulima, wafugaji, na wavuvi.



copyright© VPO-EBARR Project



copyright© VPO-EBARR Project



copyright© VPO-EBARR Project

## Lengo la mradi

Lengo la Mradi ni kuongeza uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika jamii za vijijini kwa kuimarisha mifumoikolojia na shughuli mbadal za kujiongezea kipato.

## Malengo mahsusini

1. Kujenga uwezo wa Wadau kuhusu njia na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia Mifumoikolojia (Ecosystem-based Adaptation).
2. Kuimarisha uwezo wa jamii kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kuimarisha mifumo ikolojia na kupunguza umaskini kupitia: kilimo/ufugaji kinachohimili mabadiliko ya tabianchi (Climate Smart Agriculture); shughuli mbadala za kujiongezea kipato; upatikanaji wa maji; matumizi ya majiko banifu; hifadhi ya misitu na upandaji miti na kuongoa maeneo yaliyoharibika na nyanda za malisho.
3. Kuimarisha upatikanaji wa taarifa na elimu kwa umma kuhusu mbinu bora za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mifumo ikolojia.



copyright© VPO-EBARR Project

## Shughuli zinazotekelzeza katika Maeneo ya Mradi

Shughuli za Mradi zimegawanyika kulingana na malengo kama ifutavyo:

Lengo	Shughuli za Mradi
1. Kujenga uwezo wa Wadau kuhusu mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.	<ul style="list-style-type: none"> <li>Mafunzo kwa Wataalam, wa Wizara na Halmashauri za Wilaya, Kamati za Mazingira, Vikundi vyta uzalishaji na jamii katika maeneo ya Mradi kuhusu njia na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mifumo ikolojia (ecosystem - based adaptation - EbA).</li> </ul>
2. Kuimarisha uwezo wa jamii kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi	<ul style="list-style-type: none"> <li>Mpango wa matumizi ya ardhi katika Vijiji 17 vya mradi katika Wilaya za Kishapu, Mpwapwa, Mvomero, Simanjiro na Kaskazini A.</li> <li>Kuhakikisha Upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, kilimo na mifugo kwa: Kuchimba visima virefu --&gt; Kuchimba Malambo Kishapu (2), Simanjiro (2) Mvomero (1) na Mpwapwa (2); na Ujenzi wa skimu ya umwagiliaji Lukenge Mvomero.</li> <li>Kuanzishwa kwa mashamba darasa ya Alizeti (Simajiro), Korosho (Mvomero na Mpwapwa), na Mkonge (Kishapu) na Kilimo cha mbogamboga katika Wilaya zote za Mradi; na Kuanzisha na kuwezesha shughuli za ufugaji Ng'ombe, Mbuzi, Kuku na Samaki.</li> <li>Kuanzisha viwanda vidogo vya kuongeza thamani ya mazao. Viwanda 2 vya bidhaa za ngozi Kishapu (1) Simanjiro (1); na Kiwanda cha kukamua mafuta ya Alizeti Mpwapwa.</li> <li>Kuanzisha vitalu vya miche ya miti na Utunzaji wa Misitu na shughuli za Ufugaji Nyuki katika maeneo yote ya mradi.</li> <li>Uongoaji wa maeneo yaliyoharibika vya vyanzo vya maji na nyanda za malisho.</li> <li>Kuhamasisha na kuwezesha Matumizi ya majiko banifu kupunguza ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa.</li> </ul>
3. Kuimarisha upatikanaji wa taarifa na elimu kwa umma kuhusu mbinu bora za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kuanzishwa kwa Mfumo wa kielektroniki wa taarifa na elimu kwa umma.</li> <li>Utoaji elimu kupitia machapisho, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.</li> <li>Tathmini na Ufutiliaji</li> </ul>

**Kwa mawasiliano:**  
**Katibu Mkuu,**  
**Ofisi ya Makamu wa Rais,**  
**Mji wa Serikali – Mtumba,**  
**S.L.P 2502, 40406 DODOMA**  
**(255) (22) 2163400-19 | (255) (75) 6140140**  
**ps@vpo.go.tz**



Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi  
kwa Kutumia Mifumoikolojia Vijiji  
(Ecosystem - based Adaptation for Rural  
Resilience (EBARR) in Tanzania)

